

Watu wafanye nini iwapo wamelazimishwa kufunga ndoa na mtu wasiyemtaka?

By SW - Melkisedeck Shine · April 16, 2022

Ujana na Makuzi | Mapenzi na Ngono Salama

Iwapo mtu amelazimishwa kuingia katika hali ya ndoa (kuoa/kuolewa) na msichana/mvulana ambaye hampendi, hatua ya kwanza ni kukataa ndoa hiyo na kuonyesha wazi wazi. Jadiliana suala hili na wazazi wako. Waeleze kwa heshima kwa nini hukubaliani na ndoa hiyo.

Kwa kawaida wazazi wanape-nda mambo mema kwa watoto wao. Kwa hiyo kuwepo na uhusiano mzuri kati ya wazazi na watoto kunaweza kukapangilia mambo yakaenda vizuri. Iwapo jaribio la kuzungumza na wazazi wako halikufaulu, unaweza ukazungumza na mtu mwingine unayemwamini ambaye atakubali kuzungumza na wazazi wako. Kumbuka kwamba iwapo bado unalazimishwa kufunga ndoa, unaweza kutoa taarifa polisi kwa kuwa sheria ya Tanzania hairuhusu kulazimisha ndoa.

Printable AckySHINE Article · <https://ackyshine.com/post.php?post=25668>